TANGAZO LA SERIKALI NA. 892 la tarehe 15/12/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA ADA NA VIBALI VYA BURUDANI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.

`

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

“ada” maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

”afisa mwidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

“eneo la burudani” ni mahali popote ambapo shughuli ya burudani inafanyika;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga;

“kibali cha burudani” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri; kwa ajili ya shughuli za burudani;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"shughuli ya burudani" maana yake ni sherehe, shughuli yoyote ile ya kijamii,sanaa na utamaduni, michezo na muziki.

Wajibu wa kuwa na kibali

4.-(1) Mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli ya burudani katika eneo la Halmashauri anapaswa kuwa na kibali cha maandishi kitakachotolewa na Halmashauri.

(2) Maombi yote ya vibali yatalipiwa ada kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Utaratibu wa kuomba kibali

5.-(1) Mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli ya burudani katika eneo la Halmashauri anapaswa kuwasilisha maombi ya kibali kwa Mkurugenzi kupitia kwa Afisa Mtendaji.

(2) Maombi chini ya aya ndogo ya (1) yatafanywa kupitia Fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili

(3) Iwapo maombi ya kibali yatakataliwa, Halmashauri itamtaarifu mwombaji kwa maandishi na kutoa sababu za kukataa maombi ya kibali.

(4) Mtu yeyote atakayepata kibali cha kufanya shughuli za burudani atapaswa kupeleka nakala ya kibali hicho kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ikiwa na kiambatanisho cha stakabadhi ya malipo ya ada.

Wajibu wa mmiliki wa ukumbi

6.-(1) Kila mmiliki wa ukumbi wa muziki, burudani au baa atakuwa na wajibu wa:

(a) kupiga muziki kwa kiwango cha sauti cha kawaida bila kuathiri watu wanaozunguka eneo la ukumbi huo wa muziki ;

(b) kuhakikisha wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane haingii katika kumbi hizo na endapo itabainika kuingia kwa wanafunzi au watoto mmiliki wa kumbi

atakuwa ametenda kosa.

(2) Kila mwonesha picha mjongeo au sinema atatakiwa kuweka sauti ya chini wakati wa onesho bila kuathiri majirani wanaomzunguka.

Vigezo vya utoaji kibali

7.-(1) Halmashauri itatoa kibali iwapo itajiridhisha na mambo yafuatayo:

(a) shughuli ya burudani inayoombewa kibali haitasababisha uvunjifu wa amani;
(b) eneo linaloombewa kibali cha kufanya shughuli ya burudani linaruhusiwa kwa shughuli inayoombewa kibali; na
(c) kumbi za burudani zina usalama wa kutosha ikiwa ni pamoja na kuwepo madirisha ya kutosha ya kuingiza na kutolea hewa, milango ya dharura, umeme na milango inayofunguka kwa urahisi wakati wa dharura.

(2) Muda wa burudani utakuwa ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 6:00 usiku.

Marufuku

8.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa:

(a) watoto na wanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane kuruhusiwa kuingia kwenye sehemu za starehe baada ya muda ulioruhusiwa kwisha au kulingana na sheria;
(b) mwenye ukumbi wa picha mjongeo na sinema au sehemu yoyote kuonesha picha za mjongeo ambazo hazina maadili;
(c) mwanafunzi au mtoto chini ya umri wa miaka kumi na nane kukutwa wakati wa usiku kwenye muziki au kigodoro na endapo mwanafunzi au mtoto akikutwa, mwanafunzi au mtoto na mzazi watawajibishwa kwa mujibu wa Sheria

Ndogo hii.

(2) Muda wa kuonesha picha mjongeo au sinema utaanzia saa kumi kamili jioni hadi saa sita usiku kwa siku za kazi, isipokuwa jumamosi na jumapili na siku za sikukuu itakuwa kuanzia saa saba mchana hadi saa kumi na mbili jioni.

Mmamlaka ya kufanya ukaguzi

9.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia mahala popote panapofanyika shughuli ya burudani au anapoamini kuna shughuli ya burudani inafanyika muda wowote kwa lengo la kukagua iwapo shughuli hiyo ina kibali au inafuata masharti ya kibali kulingana na Sheria Ndogo hii.

(2) Katika kutekeleza mamlaka yake chini ya aya ndogo ya (1), afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutoa maelekezo yoyote ikiwa ni pamoja na kusitisha shughuli ya burudani kulingana na hali itakayobainika baada ya ukaguzi kufanyika.

Mkusanyiko wa watoto

10.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukusanya watoto kwa ajili ya shughuli yoyote ile ndani ya Halmashauri bila kibali cha maandishi cha Halmashauri.

(2) Mkusanyiko wowote wa watoto uliopata kibali cha Halmashauri kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) utafanyika siku za mapumziko na utaanza saa nne kamili asubuhi na utamalizika kabla ya saa kumi na mbili jioni.

(3) Mtu yeyote aliyepata kibali cha mkusanyiko wa watoto atakuwa na wajibu wa kuhakikisha usalama wao kipindi chote cha mkusanyiko huo na kuhakikisha wanatawanyika kwa usalama kutoka katika eneo la mkusanyiko.

(4) Itakuwa ni makosa kwa mzazi, mlezi au mtu yeyote mwenye mamlaka juu ya mtoto kuruhusu au kusababisha kwa uzembe mtoto kuhudhuria mkusanyiko

usio na kibali cha Halmashauri.

Vibali visivyotozwa ada

11. Mikusanyiko ifuatayo itaombewa vibali bila kulipa ada:

(a) mikusanyiko ya kidini;
(b) misiba na mazishi; na
(c) michezo ya watoto isiyotozwa.

Usafi wa mazingira

12.-(1) Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za burudani ndani ya mamlaka ya Halmashauri atalazimika kufanya usafi ndani au nje ya eneo lililotumika katika shughuli ya burudani kwa kuondoa uchafu wote uliosababishwa na shughuli ya burudani.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya aya ndogo ya (1) atalipa gharama ya uchafuzi wa mazingira kadri zitakavyokadiriwa na Halmashauri na gharama zingine ambazo Halmashauri itaingia katika kuondoa uchafu huo.

Muziki unaoleta kero

13. Mtu yeyote aliyepata leseni ya biashara haruhusiwi kupiga muziki unaoleta kero kwa majirani na jamii kwa ujumla kwenye eneo lake la biashara.

Ukamataji wa vifaa

14.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata vifaa vyovyote vitakavyokutwa katika shughuli ya burudani ambayo haina kibali au inayoendeshwa bila kuzingatia masharti ya kibali.

(2) Vifaa vitakavyokamatwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) vitachukuliwa na kuhifadhiwa katika ofisi za Halmashauri au eneo lolote litakaloamuliwa na Halmashauri.

(3) Vifaa vilivyokamatwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitatakiwa kukombolewa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kukamatwa na baada ya hapo Halmashauri inaweza kuuza vifaa hivyo kwa mnada baada

ya kuomba na kupata kibali cha Mahakama.

(4) Mtu yeyote anayetaka kurejeshewa vifaa vilivyokamatwa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa gharama za ukamataji, usafirishaji na ulinzi.

Makosa na adhabu

15. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na endapo akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

16. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(2))*

ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA BURUDANI

| Namba | Aina ya Shughuli | Kiwango cha Ada kwa Shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Muziki wa Dansi, disko, taarabu na aina nyingineyo yoyote ya muziki | 50,000/= kwa siku |
| 2. | Shindano la kutafuta msanii | 30,000/= kwa shindano |
| 3. | Shindano la kutafuta warembo | 50,000/= kwa shindano |
| 4. | Maonesho ya mavazi | 50,000/= kwa onesho |
| 5. | Maombi ya kibali cha sherehe za unyago, ngoma, harusi na sherehe nyingine yoyote | 30,000/= kwa sherehe |
| 6. | Kupiga picha mjongeo | 10,000/= kwa kila tukio |
| | Mashindano ya mpira | 10,000/= kwa mechi |
| | Matangazo ya Biashara | 30,000/= kwa siku |

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 5(2))*

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI

SEHEMU YA KWANZA

(Taarifa za Mwombaji)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la mwombaji ............................................................ | 2. Anwani ya mwombaji ........................................ |
| 3. Aina ya shughuli ............................................................. | 4. Eneo analokusudia kufanya shughuli ............................................ |
| 5. Muda wa kuanza ............................................................ | 6. Muda wa kumaliza ..................................................... |
| 7. Ada ya kibali (Shilingi) ......................................................... | 8. Namba ya Stakabadhi ya malipo ................................................ |
| 9. Saini……………………………… | 10. Tarehe………………….... |

SEHEMU YA PILI
(Kwa Matumizi ya Ofisi tu)

| | |
|---|---|
| 1. Maombi namba .................................... | 2. Ada ya kibali shilingi ...................................................... |
| 3. Namba ya stakabadhi ya malipo ................................................. | 4. Tarehe ya malipo ...................................... |
| 5. Jina la Afisa aliyepokea malipo .................................................. | 6. Saini ...................................... |
| 7. Muhuri | |

Maoni ya Afisa Mwidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali (*futa isiyohusika*)
Sababu: ……………………………..…………………………………………

Jina:………………………………Saini: ……………Tarehe………………..

**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 16)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ya Mwaka 2023.
Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.
Leo tarehe …………………..ya Mwezi …………… Mwaka …………………
Jina: ………………………………………….
Saini: …………………………….

MBELE YA:
Jina: …………………………………
Wadhifa: …………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ………………………… …